JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# HOTUBA YA MHESHIMIWA KHAMIS HAMZA KHAMIS NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA

## WAKATI WA UZINDUZI WA MAONESHO YA TAASISI UWANJA WA MNAZI MMOJA, DAR ES SALAAM TAREHE 18 APRILI, 2024

APRILI, 2024

Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar;
Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi);
Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira);
Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
Mheshimiwa Edward Jonas Mpogolo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala
Wakuu wa Wilaya waliopo hapa;
Dkt. Islam Seif Salum, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa;
Mejimenti ya Ofisi ya Makamu wa Rais;
Wakurugenzi wa Wizara, Taasisi na Idara za Serikali;
Wakuu wa Taasisi za Muungano;
Washiriki wa Maonesho;
Ndugu Wananchi;
Mabibi na Mabwana.

'Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi Iendelee'.

Assalam Aleikum,

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma ambaye ametujalia afya njema na kuweza kutukutanisha hapa katika shughuli hii adhimu ya kuzindua maonesho ya Taasisi za Muungano kuelekea miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Maonesho haya ni mfululizo wa

shughuli mbalimbali zinazoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kutoa elimu ya Muungano kwa makundi mbalimbali wakiwemo Wananchi, Wabunge, Viongozi wa Serikali, Wanafunzi pamoja na makundi mengine. Napenda kukutaarifu kuwa mwitikio wa washiriki wa maonesho umekuwa mkubwa.

Aidha, Mheshimiwa Selemani Said Jafo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, alitamani sana kuja kuungana nawe katika ufunguzi wa maonesho haya lakini kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yanayomkabili amenituma nije kutoa salamu kwa niaba yake

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi***;

utakumbuka kuwa uzinduzi wa maonesho kama haya ulifanyika Zanzibar tarehe 14 Aprili, 2024 shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi kwa hotuba yake ambapo aliweka wazi umuhimu wa Muungano wetu na fursa tulizonazo sisi wananchi wa pande zote mbili za Muungano na leo tena tunazindua hapa Dar es salaam Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kwa hakika utamaduni huu ni kielelezo tosha ya mshikamano na uhusiano mzuri baina ya pandembili ili kuendelea kudumisha Muungano wetu adhimu.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi***;

Kama mnavyofahamu Ofisi ya Makamu wa Rais ( Muungano na Mazingira) ndio yenye dhamana ya Masuala ya Muungano, Ofisi hii ilianzishwa miaka 60 iliyopita, hivyo sambamba na maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano

ya Tanganyika na Zanzibar nayo Ofisi ya Makamu wa Rais itatimiza Miaka 60 mwezi Aprili mwaka huu tangu kuanzishwa kwake mwaka 1964.

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi*;

Tunapoadhimisha miaka 60 ya Muungano wetu, Watanzania wote tuna kila sababu ya kutafakari na kutathmini masuala muhimu yaliyokusudiwa na Waasisi wa Taifa letu  Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume ambao walitia saini Hati ya Makubaliano ya Muungano kwa niaba ya wananchi wa nchi hizi mbili. Pamoja na Waasisi wetu kutangulia mbele ya haki, misingi waliyotuachia imeendelea kuimarisha umoja, amani, na utulivu wa Taifa letu. Tumuombe Mwenyezi Mungu awapumzishe mahali pema peponi, Amina.

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi*;

Kama tunavyokumbuka, Tanganyika na Zanzibar zilipoungana tuliainisha mambo ishirini na mbili (22). Hivyo, kupitia maonesho haya wananchi watapata fursa ya kufahamu huduma zinazotolewa na Taasisi za Muungano, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano na pia kupata fursa ya kutoa maoni na ushauri utakaowezwsha kuimarisha na kudumisha muungano wetu. Kwa kipekee  na cha kufurahisha utafahamu chimbuko, msingi na maendeleo ya Muungano wetu uliodumu kwa miaka 60 sasa.

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi*;

Watanzania tunafurahia Muungano huu umetuletea mafanikio mbalimbali katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kwa wananchi pande zote mbili za Muungano. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na uhuru wa kuishi kwa amani na utulivu sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii bila bughudha yoyote.

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi*;

Uchumi umeimarika kutokana na mazingira na mahusiano mazuri ya kibiashara kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Aidha, tumeshuhudia kuimarika kwa miundombinu, hususan ya barabara na huduma za jamii ikiwamo afya, maji na elimu. Aidha, katika kuhakikisha usawa wa utoaji wa huduma kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano, Taasisi za Muungano zilizopo Tanzania Bara zimefungua Ofisi Zanzibar ambapo hadi sasa Taasisi 33 zimefungua Ofisi Zanzibar kati ya Taasisi 39 za Muungano. Leo tutashuhudia maonesho ya Taasisi hizo hapa Zanzibar.

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi*;

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimeendelea kuchukua hatua madhubuti za kutafutia ufumbuzi wa changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Kuanzia mwaka 2006 hadi 2024, hoja 25 zilipokelewa na kujadiliwa ambapo kati ya hoja hizo, hoja 22 zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za Muungano. Aidha, hoja zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za kupatiwa

ufumbuzi na ni Imani yangu kuwa, kwa utashi na dhamira ya dhati ya pande zote mbili, hoja zilizobaki zitapatiwa ufumbuzi.

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi*;

Katika kipindi cha miaka mitatu, 2021 hadi 2024 hoja 15 zimepatiwa ufumbuzi kati ya hoja 18 zilizokuwepo. Utatuzi wa changamoto za Muungano umeongeza imani ya Watanzania kwa Serikali zetu na hivyo kuimarisha, kudumisha amani ya muda mrefu na utulivu wa Tanzania ambao ni Tunu muhimu na fahari ya nchi yetu. Kwa namna na umuhimu wa kipekee, naomba nitoe shukrani zangu za dhati viongozi wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mhe Dr. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambao wameendeleza kwa vitendo Mawazo na fikra za waasisi wa Muungano.

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi*;

Sote tuna wajibu wa kujivunia Muungano huu na kuuendeleza kwa manufaa yetu sote kwani ni Tunu adimu na adhimu inayopaswa kulindwa kwa gharama yoyote. Tutembee kifua mbele. Wakati tunaanza shamrashamra za sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano, tushirikiane kwa pamoja kuzifanikisha sherehe hizi kulingana na mipango na ratiba zilikazoandaliwa

***"MIAKA 60 YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: TUMESHIKAMANA NA TUMEIMARIKA KWA MAENDELEO YA TAIFA LETU"***

Baada ya kusema hayo, sasa naomba kumkaribisha Mgeni rasmi ili atuzindulie maonesho hayo na kuongea na wananchi.